Swahili

# Mtoto wa kike wa mfalme na njegere

- Hadithi kutoka Denmark






Hapo zamani za kale kulikuwa na mtoto wa kiume wa mfalme. Aliyekuwa na nia ya kuoa mtoto wa kike wa kifalme, lakini ilibidi awe ametoka kwenye familia ya kifalme ya kweli. Hivyo alisafiri  na kuzunguka dunia yote  akitafuta, lakini kila sehemu hapakuwa na mtu wa kuoana nae.



Kulikuwa na watoto wa kike wa kifalme wengi, lakini hakuweza kujua kama walikuwa kweli ni watoto wa  wakike wa  kifalme, kila wakati kulikuwa na jambo ambalo halikuwa sawa. Hivyo alirudi nyumbani huku akiwa analia sana, kwa kuwa yeye alikuwa na nia ya kumpata mtoto wa kike wa mfalme(binti mfalme) wa kweli kabisa.



Siku moja palikuwa na hali ya hewa mbaya sana iliyokuwa na mvua nyingi zikiambatana na radi kali, katika lango kuu la mji kulikuwa na mtu anagonga hodi. Yule mfalme mzee alikwenda kufungua. Alikuwa ni mtoto wa kike wa mfalme amesimama nje ya mlango.




Alikuwa amelowa na mchafu kutokana na mvua zilizokuwa zinanyesha na maji ya mvua yalishuka chini ya nguo zake na kutoka nje ya viatu vyake.



“Sawa labda tutagundua” alifikiria yule malkia mzee. Malkia hakusema kitu , lakini alikwenda kwenye chumba cha kulala na kuacha njegere chini ya kitanda. Baada ya hapo alichukua magodoro ishirini (makumi mawili) na mashuka na kuyaweka juu ya njegere. Hapo ndipo atalala mtoto wa kike wa mfalme.


ZZzzz



Asubuhi mfalme na malkia walimuuliza amelalaje. “Ah vibaya tu!” alisema mtoto wa kike wa mfalme, “karibia sijaweza kulala usiku mzima”. Inaonekana palikuwa na kitu kwenye godoro. Nimelala kwenye kitu kigumu, hivyo nimekuwa wa rangi ya njano na bluu mwili mzima! Ni vibaya sana. Hivyo waliona huyu ni mtoto wa kike wa mfalme wa kweli kabisa, pamoja na kuwa amelala kwenye magodoro ishirini (makumi mawili) na mashuka ameweza kutambua kulikuwa na njegere chini.



Ni mtoto wa kike wa mfalme pekee anaeweza kutambua. Mtoto wa kiume wa mfalme akamuoa na kuwa mke wake kwa kuwa alijua kuwa huyu ni mtoto wa mfalme wa kweli.




Na njegere iliwekwa kwenye sehemu ya maonesho ambapo bado itaonekana ikiwa hakuna mtu atakaeichukua. Na huo ndo mwisho wa hadithi yetu.

**NAFO**

Nasjonalt senter for flerkulturell opplæring







Finn flere fortellinger på [morsmal.oslomet.no](http://morsmal.oslomet.no)

Fortellingen er laget med figurer og tegninger fra Aursmoen barnehage